



CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII, KILIMO NA MIFUGO (TRACDI)

S.L.P 11077, Dodoma - Tanzania

Barua Pepe: admission@tracdi.ac.tz , info@tracdi.ac.tz

Tovuti: www.tracdi.ac.tz

Simu: +255 769 479835, +255 786 829290, +255 759 275404



MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO KWA NGAZI YA STASHAHADA - 2019/2020

Ndugu, **ALI SHAABAN ALI**

TRACDI inayofuraha kukupongeza na kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya **KILIMO NA MIFUGO** ngazi ya **Stashahada**. Masomo yataanza tarehe **16/09/2019** hivyo unashauriwa kufika chuoni kabla ya tarehe hiyo. Kuchaguliwa kwako kunatokana na jitihada, mafanikio yako kitaaluma, nidhamu, kujituma na ushirikiano uliounyesha katika kufanikisha malengo katika maeneo mbalimbali ulikokuwa ukiwajibika kabla ya kuchaguliwa kujiunga chuo hiki. Ni matarajio yetu kuwa uwapo Chuoni hapa, utafanya vizuri zaidi katika taaluma na maeneo mbalimbali utakayopangiwa kuwajibika ukishirikiana na wenzio.

Chuo kipo katika Manispaa ya Dodoma eneo la Nanenane - Nzuguni. Kinajulikana kwa jina la TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE (TRACDI). Chuo kina usajili kamili wa NACTE kwa namba **REG/PWF/041**. Pia chuo kimesajiliwa na VETA kwa nambari ya usajiri **VET/DOM/PR/2015/C/040**.

A. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

i. VYETI NA VITAMBULISHO

Wakati wa **usajili utaonesha** Vyeti halisi. Baada ya uhakiki vivuli vya vyeti halisi vitabakia kwenye ofisi ya msajili.

ii. JEDWALI LINALOONESHA ADA NA MICHANGO MINGINE YA MWANAFUNZI

Course Selected		Diploma in General Agriculture
1.	Tuition Fees (Per year)	890,000
2.	Accommodation Fee (Per year)	FREE
3.	Library Fee	30,000
4.	Student Identity Card	5,000
5.	Examination Fee	15,000
6.	Institute Development Fee (Per year)	30,000
7.	Application Fee	10,000
8.	Registration Fee	5,000
9.	NACTE Quality Assurance Fee	20,000
10.	Student's Organization Fee	5,000
11.	Practical Fee	100,000
12.	Medical Fee	25,000
TOTAL		1,170,000

JINSI YA KUFANYA MALIPO

- Ili kuepukana na karaha za kusafiri na michango ya fedha kibindoni malipo yote ya michango iliyooneshwa hapo juu kwenye jedwali yatalipwa kupitia Benki mojawapo kati hizi:-
- CRDB Bank Jina la akaunti TRACDI No. 0150221739000
- TPB Bank TRACDI Account No. 223207000001
- NMB Bank Jina la akaunti TRACDI No. 52010009005
- Umoja wa wanafunzi (TSH 5,000) CRDB Bank jina la akaunti TRACDISO No. 0152219156100

NACTE ADMISSION FEE

After all the procedures of application, the applicant is required to make payments of Tsh 20,000/= as NACTE Admission Fee through TPB bank by using M-pesa, Tigo pesa and Airtel Money. Instruction for payments (Maelekezo ya jinsi ya kulipa)

M-PESA

1. Piga: *150*00#
2. Chagua namba 4. Weka namba ya kampuni
3. Weka namba ya kampuni 700500
4. Weka namba ya kumbu kumbu 9990769120050
5. Weka kiasi (20,400)
6. Weka namba ya siri ****
7. Bonyeza 1 kuthibitisha

Mitandao mingine fanya malipo kwa kufuata mfano hapo juu kulingana na kampuni ya mtandao unaotumia au lipa katika akaunti za benki zilizoordheshwa hapo juu.

- **Angalizo:** Wanafunzi wote wanajitegemea chakula kwa kupika au kujinunulia mgahawani. Gharama kadiliwa ni Sh. 2,500 kwa siku endapo ana nunua chakula na nipungufu kwa wanaojipikia.
- Pia mwanafunzi aje na Koti maalumu litakalovaliwa anapoingia maabara (**Labcot**) na kofia yake vyote rangi nyeupe, Viatu maalum kwa ajili ya shughuli za shamba (**Gambut**) na Vazi la **Overall** litalovaliwa wakati awapo shambani pamoja na jembe na mpini wake.

Michango hii inatakiwa kulipwa kwa pesa tasilimu pindi mwanafunzi anaporipoti chuoni kwa ajili ya usajili.

B. MAHITAJI MAALUMU KWA MWANAFUNZI

(i) MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI

1. Shuka 2
2. Mto wenye foronya
3. Godoro ndogo upana futi mbili na nusu (2.5) na urefu futi 6 pamoja na Chandarua

(ii) MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA

1. Fyekeo
2. Reki
3. Jembe
4. Water Cane
5. Knapsack Sprayer
6. Ream mbili A4
7. Daftari kubwa (counter books) kwa nukuu zako za masomo
8. Faili mbili za kutunzia nyaraka za Mwanafunzi (File Box)

Pia mahitaji haya yanapatikana hapa Dodoma hiyo tunamshauri mwanafunzi ikiwezekana anunulie hapa kupunguza mizigo.

UTAKAPOKUWA HAPA CHUONI UTAFAHAMISHWA JUU YA SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO. AIDHA, UTAPEWA MAFUNZO KARIBISHI (ORIENTATION) NA FOMU YA KUJAZA KUKUBALIANA NA SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO.

Karibu TRACDI



ASHA SEYA
MKUU WA CHUO